SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 20 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) OKTOBA 2022

WAZIRI BASHUNGWA AMTEUA NA KUMWAPISHA FELISTER SHULI KUWA MJUMBE WA TSC

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) akimwapisha Bibi Felister Emmanuel Shuli kuwa Kamishna wa TSC katika hafla iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa OR – TAMISEMI jijini Dodoma Septemba 29, 2022.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

HONGERA SERIKALI KWA KUTENGA BILIONI 55.57 KWA AJILI YA KUJENGA NYUMBA ZA WALIMU

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi makini wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuboresha mazingira ya walimu na Sekta ya Elimu kwa ujumla.

Tukiachilia mbali masula ya upandishwaji vyeo/madaraja ya walimu ambapo kwa sasa hakuna tena malalamiko ya kukaa kwenye cheo kimoja kwa muda mrefu kinyume na taratibu, Rais Samia aliamua kupeleka fedha nyingi katika ujenzi wa madarasa na sasa tunashuhudia wanafunzi wanasoma wakiwa katika mazingira mazuri na hata walimu wanapata hamasa ya kufundisha wanafunzi wakiwa na utulivu darasani.

Kama hiyo haitoshi, hivi karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa amekaririwa akisema kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 55.57 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 809 zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua kaya 1916.

Uamuzi huu wa Serikali umekuja wakati mwafaka ambapo moja ya changamoto zinazowakabili walimu ni kukosa nyumba za kuishi karibu na shule hususan katika maeneo ya vijijini. Tunaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoonesha dhamira ya dhati ya Rais Samia katika kuwajali na kuwathamini walimu hapa nchini.

Bila shaka, kila mwalimu anaona namna Serikali inavyojitahidi kuweka mazingira bora ili wanafunzi waweze kupewa huduma stahiki. Matarajio ya Serikali ni kuwa kila mwalimu atajitahidi kutimiza wajibu wake na kutojihusisha na masuala mbalimbali yanayorudisha nyuma maendeleo na ndoto za wanafunzi wetu.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina Nkwama

Wajumbe
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

Mhariri Mkuu
Gerard Chami

Mhariri
Adili Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

WAZIRI BASHUNGWA AMTEUA NA KUMWAPISHA FELISTER SHULI KUWA MJUMBE WA TSC

Bibi Felister Emmanuel Shuli (kulia) kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akila kiapo cha kuwa Kamishna wa TSC mbele ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) Septemba 29, 2022 jijini Dodoma.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Innocent Bashungwa amemteua na kumwapisha Bibi. Felister Emmanuel Shuli kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Mathew Kirama ambaye aliteuliwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma na hivyo kupoteza sifa ya kuendelea kuwa mjumbe TSC kwa mujibu wa Sheria.

Katika hafla ya uapisho huo iliyofanyika Septemba 29, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa OR – TAMISEMI, Waziri Bashungwa alimpongeza Shuli kwa kuteuliwa ambapo anaungana na Wajumbe wengine walioteuliwa mnamo tarehe 18 Mei, 2020.

"Naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Bibi Felister E. Shuli Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu ambaye nimemteua na kumuapisha leo hii. Pia niwapongeze Mwenyekiti wa Tume na Wajumbe wengine saba (7) ambao waliteuliwa awali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi," alisema Waziri Bashungwa.

Waziri huyo alieleza kuwa kuteuliwa kwa Shuli pamoja na wajumbe wengine wa Tume, kunatokana na Mamlaka ya Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI chini ya Kifungu cha 6(1)(b) kinachompa uwezo wa kuteua wajumbe

Bibi Felister Emmanuel Shuli (kulia) kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akisaini hati ya kiapo baada ya kuapishwa kuwa Kamishna wa TSC mbele ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) Septemba 29, 2022 jijini Dodoma.

nane (8) kutoka kwenye Taasisi za Umma na Chama cha Walimu Tanzania.

Alieleza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu ina majukumu ambayo yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria Na. 25 ya mwaka 2015 iliyoanzisha Tume na Kanuni zake za Mwaka 2016 huku akimpongeza Mwenyekiti, Katibu, Wajumbe pamoja na wafanyakazi Tume hiyo kwa jitihada wanazofanya kufikia utekelezaji wa majukumu hayo na kusaidia kupungua kwa malalamiko ya walimu.

"Pamoja na kuwapongeza, nawaomba Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa kushirikiana na Katibu muweke mikakati ya namna bora zaidi ya kutatua changamoto za Walimu zikiwemo upandishwaji vyeo, kubadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza na madai mbalimbali ya Walimu,"alisema.

Aliongeza kuwa, "nawaomba muwe chachu katika kuhakikisha kuwa changamoto zinazowakabili walimu zinatatuliwa mapema na hivyo, kufikia malengo ya kuanzishwa kwa chombo hiki. Aidha, nasisitiza Kamati za Nidhamu ngazi za Wilaya na Tume kutenda haki kwa walimu pale wajumbe wanapofanya uamuzi katika kushughulikia Mashauri ya Nidhamu."

Pamoja na hayo, Waziri Bashungwa aliitaka TSC kuhakikisha inasimamia vyema mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi hiyo huku akiahidi kufanya ziara za kustukiza kwa ajili ya kuona maendeleo ya mradi huo na kusisitiza kuwa hatavumilia uzembe wa aina yoyote unaokwamisha utekelezaji wa

WAZIRI BASHUNGWA AMTEUA NA KUMWAPISHA FELISTER SHULI KUWA MJUMBE WA TSC

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) akisaini hati ya kiapo mara baada ya kumwapisha Bibi Felister Emmanuel Shuli (kulia) kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwa Kamishna wa TSC.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) akimlabidhi Kamishna mpya wa TSC, Felister Emmanuel Shuli vyenzo za kazi wakati wa hafla ya kuapishwa kwa kamishna huyo iliyofanyika Septemba 29, 2022 jijini Dodoma.

WAZIRI BASHUNGWA AMTEUA NA KUMWAPISHA FELISTER SHULI KUWA MJUMBE WA TSC

Kamishna Mpya wa TSC kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bibi Felister Emmanuel Shuli.

mradi.

"Hakikisheni fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa jengo la ofisi zinatumika vizuri. Nina imani kuwa shughuli za ujenzi zinakwenda vizuri, muda wowote nitafanya ziara kuona namna utekelezaji wa mradi huo unavyokwenda. Lakini niseme tu kwamba sitakuwa tayari kuoana aina yoyote ya uzembe unaolenga kukwamisha utekelezaji wa mradi huo kama ulivyopangwa," alisema Bashungwa.

Awali, akitoa neno la kumkaribisha Waziri huyo, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Lazaro Komba alisema kuteuliwa na kuapishwa kwa mjumbe huyo kunakamilisha safu ya wajumbe wa TSC waliotajwa kwenye Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448.

Aliongeza kuwa muundo wa Tume hiyo umewekwa kimkakati kwa kuzingatia unyeti wake na aina ya majukumu yanayotekelezwa na ofisi hiyo ambapo alisema kamishna kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kiungo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Tume kwani Wizara hiyo ndiyo inayotoa miongozo mbalimbali inayohusu utumishi wa Umma.

Kwa upande wake Bibi Shuli alishukuru kwa kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi hiyo huku akieleza kuwa atatumia uwezo na uzoefu wake katika kusaidia TSC kufikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kama inavyoelekezwa na sheria iliyoanzisha Tume hiyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) akiongea na Menejimenti ya TSC pamoja na Vyombo vya habari mara baada ya kumwapisha Kamishna mpya wa TSC, Bibi Felister Shuli hivi karibuni jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa neno la utangulizi kwa ajili ya kumkaribisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) wakati wa hafla ya kumwapisha Kamishna mpya wa TSC, Bibi Felister Shuli.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) akiongea na Menejimenti ya TSC pamoja na Vyombo vya habari mara baada ya kumwapisha Kamishna mpya wa TSC, Bibi Felister Shuli hivi karibuni jijini Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Katibu Mkuu (Elimu) wa OR TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde (wa pili kulia), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia) pamoja na Kamishna wa TSC, Felister Shuli.

Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati) akiwa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) wakimkaribisha Kamishna mpya wa TSC, Felister Shuli (kulia) katika ofisi za TSC Makao Makuu, Dodoma.

Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi juu ya maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya TSC Makao Makuu kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) wakati wa hafla ya kumwapisha Kamishna mpya wa TSC, Bibi Felister Shuli hivi karibuni jijini Dodoma. Pichani, katikati ni Naibu Katibu Mkuu wa OR – TAMISEMI anayesimamia masuala ya Elimu, Dkt. Charles Msonde.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Katibu Mkuu (Elimu) wa OR TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde (wa pili kulia), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia), Kamishna wa TSC, Felister Shuli pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC (waliosimama).

KATIBU TSC AMEWATAKA WADAU WOTE WA ELIMU KUWA NA USHIRIKIANO WA KARIBU KATIKA KUHUDUMIA WALIMU NCHINI

- Yaelekezwa Walimu waheshimiwe na kutodhalilishwa;
- Manispaa na Wazazi watakiwa kutoa huduma ya chakula shuleni;
- Ufundishaji stadi za KKK kwa madarasa ya awali wasisitizwa;
- Yaelekezwa maeneo ya shule kupimwa na kuwekewa mipaka;
- Dar yapokea Bil.21.2 ujenzi wa miundombinu ya shule; na
- Wadau watakiwa kushiriki kikamilifu utekelezaji wa miongozo.

Na. Mwandishi Wetu,
Dar Es Salaam.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama, ndc amewaomba na kuwasihi wadau wote wa sekta ya elimu nchini kuongeza na kudumisha ushirikiano wa karibu uliopo katika kuwahudumia Walimu kwa weledi na ufanisi katika maeneo yao ya kazi hapa nchini.

Alisema, lengo kuu la kusisitiza ushirikiano huu ni kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan katika kuboresha huduma za elimu nchini kwani Walimu wana malengo ambayo hujiwekea kuyatimiza kwa manufaa ya Taifa na ili kuyafikia ni lazima kwa pamoja kuwajengea ari katika kutoa huduma ya elimu kwa matokeo chanya ya wanafunzi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mwalimu Nkwama aliyasema hayo hivi karibuni kwenye hafla ya uzinduzi wa miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyofanyika Jijini Dar Es Salaam ambapo Mhe. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, alikua Mgeni Rasmi.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,Amos Makala akionesha vitabu vya miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati wa hafla ya uzinduzi wa miongozo hiyo kwa Mkoa wa Dar es Salaam uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na wadau wa Elimu wa Mkoa wa Dar es Sakaam kwenye hafla ya uzinduzi wa miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyofanyika Jijini Dar Es Salaam hivi karibuni.

KATIBU TSC AMEWATAKA WADAU WOTE WA ELIMU KUWA NA USHIRIKIANO WA KARIBU KATIKA KUHUDUMIA WALIMU NCHINI

Akiwasilisha hotuba yake Mgeni Rasmi, Mhe. Amos Makalla, alimshukuru Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuleta fedha za maendeleo katika mikoa ambapo kwa Mkoa wa Dar Es Salaam pekee hadi kufikia mwezi Septemba, 2022 jumla ya Tshs.21,168,034,782.17 zilikua zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule.

Akitambua mchango wa wadau wa sekta ya elimu nchini, Mkuu huyo wa Mkoa wa Dar Es Salaam aliwapongeza na kuwashukuru wadau wote kwa kusimamia elimu kikamilifu na kupelekea Mkoa wa Dar es Salaam kung'ara katika matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na Kidato cha Nne 2021.

"Nafahamu tumepata mafanikio mengi sana katika sekta ya elimu katika Mkoa wetu, hususan katika taaluma na michezo. Pamoja na mafanikio hayo bado zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii ya elimu katika mkoa wetu. Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliunda kikosi kazi cha kupitia changamoto zinazoikabili sekta ya elimu na kuandaa miongozo ambayo imebainisha changamoto hizo na mikakati ya kutatua changamoto na sasa tunaizindua miongozo hiyo katika Mkoa wetu." Alisema Mhe. Makalla

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto) akiwa na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyofanyika Jijini Dar Es Salaam hivi karibuni. Pichani, watatu kutoka kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala akikata utepe kuashiria uzinduzi wa miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mkoa wa Dar es Salaam uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Pamoja na uzinduzi wa Miongozo hiyo, Mhe. Makalla aliwaagiza Wakuu wote wa Wilaya Mkoani Dar Es Salaam kuhakikisha wanasimamia kikamilifu utekelezaji wa miongozo hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa huku kila Wilaya ikipitia changamoto zilizoainishwa na zilizopo kwenye maeneo yao kisha kujipanga kwa namna ya kutatua changamoto hizo.

Vile vile, Mkuu huyo wa Mkoa wa Dar Es Salaam aliwataka kusimamia kikamilifu zoezi la uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule waandikishwe na kujiunga na elimu ya awali, msingi na wale

KATIBU TSC AMEWATAKA WADAU WOTE WA ELIMU KUWA NA USHIRIKIANO WA KARIBU KATIKA KUHUDUMIA WALIMU NCHINI

wote waliofaulu darasa saba wahakikishwe wanajiunga na shule za sekondari (kidato cha kwanza) kwa mwaka 2023.

Mhe. Makalla pia aliwaagiza Wakuu wa Wilaya hao kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa miundombinu ya shule hasa vyumba vya madarasa, vyoo na ununuzi wa madawati na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anaekaa chini katika Mkoa wa Dar Es Salaam ifikapo mwezi Januari, 2023.

Aidha, aliwasisitiza kuhakikisha kunakua na usimamizi madhubuti wa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo shuleni kwani zinapaswa kutumika kama ilivyokusudiwa na sio vinginevyo na ujenzi kukamilika kwa wakati.

Pamoja na maelekezo hayo kwa Wakuu wa Wilaya, Mkuu huyo wa Mkoa alitoa maagizo kwa Maafisa Elimu wote ndani ya Mkoa wa Dar Es Salaam kuhakikisha wanasimamia kikamilifu ufundishaji wa stadi za KKK (Kusoma, Kuhesabu na Kuandika) kwa madarasa ya awali, darasa la kwanza na pili huku kukiwa hakuna mwanafunzi yoyote wa Mkoa wa Dar es Salaam ambae ataingia darasa la tatu akiwa hamudu stadi hizo.

Pia, ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki na kuboresha utoaji wa taaluma na ufaulu katika mitihami ya kitaifa, aliziagiza Manispaa zote ndani ya Mkoa huo kwa kushirikiana na wazazi kuhakikisha shule zote zinatoa huduma ya chakula cha mchana shuleni.

"Manispaa zote hakikisheni maeneo ya shule yamepimwa na kuwekewa mpaka ili kuepusha migogoro inayojitokeza mara mara kwenye shule zetu na kuleta usumbufu usio wa lazima kwa Walimu na Wanafunzi. Lakini bado Manispaa zote mnawajibika kusimamia utekelezaji wa mafunzo ya Walimu kazini kupitia kwenye vituo vya Walimu ili kubadilishana uzoefu na kujenga umahiri wa ufundishaji. Na ili kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi kwenye Shule za Sekondari, kila Halmashari ikamilishe ujenzi wa Maabara katika shule zote ili kuwezesha wanafunzi kusoma kwa vitendo." Alisema Mhe. Makalla

Alimalizia kwa kuzitaka Halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha Walimu wanaheshimiwa na hawadhalilishwi kwa namna yoyote na mtu yeyote wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao na kutaka haki zao zilindwe huku Viongozi wote wa Elimu, Maafisa Elimu, Makatibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule Msingi na Sekondari kila mmoja akitakiwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miongozo iliyozinduliwa.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Mhe. Katibu wa CCM Mkoa, Katibu Tawala Mkoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Maafisa Elimu wa Mkoa, Makatibu Tawala wa Wilaya, Ma Meya wa Jiji na Manispaa, Wakurugenzi wa Halmashauri za Manispaa, Maafisa Elimu Wilaya Msingi na Sekondari, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Maafisa wa Idara ya Elimu wa Mkoa na Manispaa na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari mkoani humo.

Wadau mbalimbali wa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa katika hafla ya uzinduzi wa miongozo ya mikakati ya uendeshaji na usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyofanyika Jijini Dar Es Salaam hivi karibuni.

WALIMU NI WATU MUHIMU SANA KATIKA MUSTAKABALI WA MAENDELEO YA TAIFA LETU – DKT. MSONDE

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akizungumza na Makamishna na Sekretarieti ya Tume wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma.

Na. Mwandishi Wetu, Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Enock Msonde, amesema Walimu ni watu muhimu sana katika mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu kwani ni watu ambao sisi sote na taaluma zote hapa nchini na duniani tunawategemea kufikia popote tunapolenga kufika.

Dkt. Msonde aliyasema hayo wakati akizungumza na Mwenyekiti, Makamishna na Sekretarieti ya Tume wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika moja ya kumbi za mikutano zilizopo Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma.

"Ili walimu waweze kutekeleza majukumu yao na kuleta matokeo chanya kwa Taifa ni lazima wapewe kipaumbele kiwanachostahili kwani ni kada muhimu sana kwa taaluma zote na tunawategemea kufikia popote tunapolenga kufika." Alisema Dkt. Msonde

Alisema kuwa kwa kipindi ambacho amepewa jukumu la kushughulika na Elimu akiwa OR-TAMISEMI amebaini kuwa morali ya kada ya Ualimu imeshuka sana na walimu wamepungukiwa hamasa ya kazi, ari ya kazi huku wajibu wa Tume ukiwa ni

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akizungumza na Makamishna na Sekretarieti ya Tume wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma.

WALIMU NI WATU MUHIMU SANA KATIKA MUSTAKABALI WA MAENDELEO YA TAIFA LETU – DKT. MSONDE

kutambua hilo na kupambana kuinua hamasa ya Walimu na ari yao iwe katika hali ya juu wakati tukitambua kuwa bila hivyo sisi sote kama Taifa hatatuwezesha kufikia malengo mapana na makubwa tunayoyategemea Walimu wayalete.

Vilevile, Naibu Katibu Mkuu huyo alisema, Walimu wamekua na sauti ya wengi kwa kila mtu kuwa ni kiongozi wa Walimu, na bahati mbaya wengi hawajui ni kitu gani unaweza kuwaambia Walimu hadharani na kipi huwezi kuwaambia hadharani, hata kama Mwalimu amekosea.

"Katika kuendeleza mazingira yetu mapya kabisa ya kumhudumia Mwalimu ni vema kulizingatia jukumu letu kubwa la kimkakati ambalo ni kuwatumikia Walimu badala ya wao kututumikia. Haya ni maelekezo katika ngazi zote kuanzia Mikoa, Halmashauri nyinginezo wote wanaotoa huduma kwa Walimu wanatakiwa kwenda kumtumikia Mwalimu katika kituo chake cha kazi. Ni marufuku mwalimu kushinda kwenye korido kutafuta haki yake na hivyo naelekeza tena kuwa Mwalimu ahudumiwe katika kituo chake cha kazi na hii ndivyo Tume inatakiwa ifanye kazi badala ya viongozi wa Tume kukaa maofisini." Alisema Naibu Katibu Mkuu (Elimu)

Mwnyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma.

Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde alipotembelea Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma.

Dkt. Msonde alisema katika kikao chake na Walimu siku za hivi karibuni alifarijika kusikia wakikiri kutokua na malalamiko wala madai ya ziada na Tume wakisadifu

WALIMU NI WATU MUHIMU SANA KATIKA MUSTAKABALI WA MAENDELEO YA TAIFA LETU – DKT. MSONDE

kuwa wana morali mpya na kubwa ya kufanya kazi kwani Tume imekua ikiwahudumia na kuwashughulikia vema na kwa wakati katika mahitaji yao yote ya msingi yanayopatikana TSC ikiwemo; kuwapandisha madaraja, kuhakikisha wanapata mishahara stahiki na kwa wakati, kupata kwa wakati vibali vya kustaafu, viongozi wa TSC kufika katika maeneo yao ya kazi na kuzungumza nao ikiwa ni pamoja na kutatua kero na mahitaji yao muhimu ambayo wangeyafuata katika Ofisi za TSC Makao Makuu na Wilayani.

Aidha, alisema pale ambapo kuna changamoto za miundombinu na vitendea kazi kwa Tume kama usafiri kufika katika vituo vya kazi vya Walimu kuwahudumia; Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeweka mazingira wezeshi ambapo imeelekeza tena viongozi wa Tume Wilayani na Halmashauri zote nchini wafanye kazi kwa ushirikiano wa pamoja bila kuwekeana mipaka isiyo

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (wa kwanza kushoto kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina M. Nkwama (kulia) pamoja na Makamishna wa TSC (waliosimama) wakati Naibu Katibu Mkuu huyo alipotembelea Mkutano wa Tume uliokuwa unaendelea jijini Dodoma.

na msingi katika utekelezaji wa majukumu na kuwataka watumie kwa pamoja magari yaliyopo wilayani kufika katika vituo vya Walimu nyakati zote na kutoa huduma bila bugudha wala urasimu kwa Walimu ambao ni tegemeo la Taifa lolote duniani.

Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma ukiwa unaendelea.

Dkt. Msonde aliongeza kuwa pamoja na kufuatilia ufundishaji wa Walimu na matokeo yao katika vituo vyao vya kazi, pia viongozi hao waangalie Walimu wana matatizo gani, kero zao zisemwe na kutafutiwa ufumbuzi wa haraka na kupewa mrejesho wa jambo husika lililowasilishwa kujua limefikia wapi iwe chanya au hasi wafahamishwe.

Hata hivyo Naibu Katibu Mkuu huyo aliahidi kuzichukua changamoto zote zilizoainishwa na kwenda kuzitafutia ufumbuzi wa pamoja kama Wizara na Taasisi nyingine za Serikali zinazohusika ikiwa ni pamoja na kuangalia namna ambavyo Tume itaweza

WALIMU NI WATU MUHIMU SANA KATIKA MUSTAKABALI WA MAENDELEO YA TAIFA LETU – DKT. MSONDE

kupata rasilimali fedha zaidi kwa ajili ya kukamilisha kwa wakati ujenzi wa jengo la Tume Makao Makuu huku akiwapongeza kwa kazi nzuri na iliyotukuka wanayofanya.

Nae Mwenyekiti wa Tume, Pro. Willy Komba, akitoa maelezo ya utangulizi kabla ya kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu (Elimu), Dkt. Charles Msonde, alisema Tume imekua na utaratibu endelevu wa kutoa elimu kwa wadau wake hasa Walimu kuhusiana na Maadili ya Kazi ya Ualimu na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu wanaokiuka maadili ya kazi.

Pamoja na hilo Prof. Komba alisema, "Tunashughulika na maendeleo ya Walimu ili waweze kufanya kazi kwa tija na ufanisi zaidi; tunawapandisha vyeo, tunawabadilisha vyeo, tunatoa vibali vya kustaafu tukishirikiana na OR-TAMISEMI kupitia Halmashauri zao husika waliko Walimu wenye uhitaji huo."

Akiyataja majukumu ya jumla ya Tume kwa Walimu hapa nchini, Mwenyekiti huyo alisema kuwa ni pamoja na kushughulikia ajira (kusajili Walimu, kuthibitisha kazini Walimu, kuajiri upya Walimu waliokaa nje ya Utumishi wa Umma kwa sababu mbalimbali), maadili (kutoa elimu kuhusiana na maadili ya kazi ya Ualimu na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu wanaokiuka Maadili ya Kazi ya Ualimu) na Maendeleo ya Walimu (kuwapandisha vyeo Walimu, kuwabadilisha vyeo Walimu wanaojiendeleza na kutoa vibali vya kustaafu).

Prof. Komba aliyataja mafanikio mbalimbali ya Tume tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa akitolea mfano kwa miaka miwili mfululizo 2020/2021 na 2021/2022 kuwa ni pamoja na; kufanyika kwa vikao vya kisheria vitatu mpaka vinne kwa ngazi ya Wilaya na Makao Makuu kama Sheria inavyoelekeza ambapo Walimu kupitia vikao hivyo wamepandishwa vyeo, wamethibitishwa kazini, wamebadilishiwa vyeo, mashauri ya nidhamu yametolewa uamuzi na rufaa zimeamuliwa.

Pamoja na mafanikio hayo alisema mafanikio mengine ni pamoja na ujenzi wa Mfumo wa Teachers Service Commission Management Information System -TSCMIS Moduli Sita zilizotakiwa kujengwa kukamilika na kuwezesha hatua ya kufanyiwa majaribio ya matumizi kuanza, kupata kiwanja na kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu, kuendelea kupata hati safi ya hesabu zilizokaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Tume kufikia hatua ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambapo ilielekezwa wadau waliojumuishwa kuhusishwa na mabadiliko ya Sheria kushiriki kwa kutoa maoni yao, kukamilisha Muundo wa Utumishi na Mishahara na kuuwasilisha OR-TAMISEMI ambapo umewasilishwa OR-MUUUB na Fungu la Tume kuendelea kuwezeshwa kupata fedha.

Mwenyekiti huyo wa Tume alisema popote palipo na mafanikio hapakosi changamoto huku akiainisha sehemu ya changamoto hizo kuwa ni pampja na; upungufu wa watumishi, kusheheni kwa maombi ya Walimu kuajiriwa upya, kutoteuliwa kwa mmoja wa Mjumbe kutimiza safu ya Wajumbe wa Tume, ujenzi

Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma ukiwa unaendelea.

WALIMU NI WATU MUHIMU SANA KATIKA MUSTAKABALI WA MAENDELEO YA TAIFA LETU – DKT. MSONDE

zisizoridhisha wa vyumba vya Ofisi Wilayani na Makao Makuu, kuchelewa kuidhinishwa kwa Muundo wa Tume unaopelekea kutoteuliwa kwa Katibu Wasaidizi Wilayani, ufinyu wa Bajeti, uchache wa vitendea kazi kama magari, compyuta za mezani, compyuta mpakato, n. k pamoja na uwepo wa Mfumo wa TSCMIS.

Akichangia maelezo ya awali ya Mwenyekiti wa Tume na kuwasilisha ombi maalumu la ushughulikia mapema maombi ya Walimu kurejea kazini baada ya kutumikia kwa mwaka mmoja adhabu za makosa yao ya awali na kuadhibiwa na Tume, Kamishna Mwl. Jane Ntindya ambaye ni mwakilishi wa Elimu Sekondari alisema Tume imekua ikiridhia mara kwa mara baadhi ya maombi ya Walimu wanaohitaji kurudi kazini kwa mujibu wa Sheria baada ya kutumikia adhabu zao kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kufanya makosa na kupewa adhabu na Tume lakini wamekua hawapati majibu ya maombi hayo kwa wakati kutokana na kutojadiliwa kwa muda stahiki na mamlaka nyingine zinazohusika na hivyo Walimu hao kupoteza malengo kwa kusubiri muda mrefu na mwisho kupoteza kabisa mwelekeo wa maisha.

Mwisho, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, alisema kuwa Kamati zote za Tume Wilayani katika kanda saba za Tume zilizopo zimeshapatiwa mafunzo ya namna ya kuendesha vikao vyao, kuijua Tume na taratibu zake, ushughulikiaji wa mashauri

Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 uliofanyika hivi karibuni katika kumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention jijini Dodoma ukiwa unaendelea.

yanayowasilishwa katika ngazi ya wilaya ambapo kati ya wajumbe watano kutoka Kamati za Wilaya ni Wajumbe Wawili na Katibu Msaidizi wa Tume Wilayani, Mwenyekiti na Mjumbe mmoja kutoka Elimu Msingi au Sekondari wamejengewa uwezo kwa kadri bajeti ilivyoruhusu.

Katibu huyo alisema bado Tume inaendelea kutoa elimu kwa kadri inavyopata fursa katika matukio na mijumuiko mbalimbali ambayo inawajumisha wadau mbalimbali wa Tume kwani kwa sehemu bado baadhi ya Walimu hawajui Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayowaongoza katika kufuatilia masuala mbalimbali yawahusuyo kitaaluma na kiutumishi.

Mwl. Nkwama alisema takribani asilimia 70 ya makosa yanayowakabili Walimu ni utoro na kukamilika vizuri kwa mwarobaini wa mawasiliano kama alivyoelekeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa kuwa hoja mbalimbali na majibu ya barua za Walimu yapatikane ndani ya siku saba badala ya kusubiri kwa muda mrefu basi haya makosa mengine yatakwisha na tutakwenda vizuri.

Katika Mkutano huo wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya rufaa za mashauri 60 ziliwasilishwa na kusikilizwa ambapo rufaa za mashauri 30 zilikataliwa kwasababu mbalimbali, rufaa za mashauri 12 zilielekezwa kuanzishwa upya, rufaa za mashauri tisa ziliwasilishwa nje ya muda na rufaa za mashauri tisa zilikubaliwa.

WADAU WA ELIMU BABATI WATAKA TSC ITOE ELIMU ZAIDI KWA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Babati.

Wadau wa Elimu wilayani Babati wameiomba Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoa elimu zaidi kwa walimu juu ya masuala mbalimbali ya kiutumishi ili kuwawezesha kufahamu haki zao na taratibu mbalimbali za kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wadau hao wametoa ombi hilo hivi karibuni wakati walipokutana na Maafisa kutoka TSC Makao Makuu waliofika wilayani hapo kwa lengo la kukusanya taarifa kwa njia ya madodoso ikiwa ni sehemu ya kufanya utafiti wa msingi (baseline survey) juu ya hali ya utumishi wa walimu nchini.

Wadau hao walieleza kuwa walimu wengi bado hawana uelewa mkubwa juu ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu kitu ambacho kinaleta changamoto ya utatuzi wa masuala mbalimbali yanayowakabili.

"Tunaomba TSC muendelee kuwafikia walimu na kuwapa elimu juu ya taratibu mbalimbali katika utumishi wao. Kwa sasa, unaweza kuona mwalimu ana shida yake lakini hajui ni chombo gani sahihi kinachopaswa kumshughulikia. Tunajua walimu wanasimamiwa na zaidi ya chombo kimoja, hivyo TSC mna wajibu wakuwaelimisha walimu kuhusu taratibu zote za utumishi," alisema mmoja wa wadau.

Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akizungumza na wadau wa elimu (hawapo pichani) hivi karibuni wilayani Babati.

Naye Afisa Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa alieleza kuwa pamoja na kwamba TSC imeendelea kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu, walimu nao hawanabudi

Afisa Utumishi Mwandamizi, Francis Gwankisa kutoka TSC Makao Makuu akizungumza na wadau wa elimu hivi karibuni wilayani Babati.

WADAU WA ELIMU BABATI WATAKA TSC ITOE ELIMU ZAIDI KWA WALIMU

Kikao cha wadau wa elimu kikiwa kinaendelea mjini Babati.

Baadhi ya wadau wa elimu wakimsikiliza Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa (hayupo pichani) wakati wa kikao chao kilichofanyika wilayani Babati hivi karibuni.

kujishughulisha kujua taratibu hizo kwa kujisomea wenyewe.

"Ni kweli kwamba tunaendelea kutoa elimu, lakini ni vyema pia kila mwalimu akafanya jitihada za ziada kujua taratibu mbalimbali za kiutumishi kwa kuwa ni kwa faida yake mwenyewe. Kwa sasa kila kitu kimewekwa wazi, mambo mengi unaweza kuyapata kwa kutumia simu yako ya mkononi. Hivyo, ninawasihi tusisubiri hadi TSC ifikike kutoa elimu, pale inapowezekana tuendelee kujisomea kuongeza uelewa," alisema Gwankisa.

Pamoja na hayo, Afisa huyo aliwasisitiza walimu kuhakikisha wanatunza nyaraka zao za kiutumishi ili pale zinapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati bila kuleta usumbufu unaosababisha kucheleweshwa kwa huduma.

Kikao hicho kifupi kiliwahusisha badhi ya walimu, wakuu wa shule, maafisa elimu, wathibiti ubora, pamoja na wananchi wa kawaida na kilifanyika baada ya wadau hao kukamilisha ujazaji wa madodoso.

Baadhi ya wadau wa elimu wakimsikiliza Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa (hayupo pichani) wakati wa kikao chao kilichofanyika wilayani Babati hivi karibuni.

MAANDALIZI YA MKUTANO WA KWANZA WA TSC KWA MWAKA 2022/2023

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiongoza kikao cha maandaizi ya Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakiwa katika Kikao cha maadndalizi ya Mkutano wa Tume. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma.

Kikao cha Menejimenti ya TSC kwa ajili ya kufanya maadalizi ya Mkutano wa Tume kikiwa kinaendelea.

Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, Evodia Pangani (wa kwanza kulia) akifafanua jambo wakati wa kikoa cha Menejimenti ya TSC kilichokaa hivi karibuni kwa ajili ya kufanya maandalizi ya Mkutano wa Tume hiyo.

TSC MPWAPWA YAFANYA ZIARA KWENYE SHULE MBALIMBALI WILAYANI HUMO

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mpwapwa, Patricia Binde akijibu hoja mbalimbali za walimu wakati wa ziara yake aliyoifanya katika Shule ya Msingi Idunda hivi karibuni.

Baadhi ya watumishi wa TSC-Mpwapwa wakiwa kwenye picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Idunda.

Mwalimu akiuliza swali wakati wa Kikao kilichowakutananisha Maafisa wa TSC Wilaya ya Mpwapwa na baabdhi ya walimu wilayani hapo. Kikao hicho kilifanyika katika Shule ya Sekondari Mpwapwa.

Majadiliano ya pamoja kuhusu changamoto mbalimbali za walimu yakiendelea katika shule ya sekondari Pwaga kati ya Walimu na maafisa wa TSC Wilaya ya Mpwapwa.

Watumishi wa TSC Wilaya ya Mpwapwa wakiwa kwenye picha ya pamoja na walimu wa shule Msingi na Sekondari Pwaga.

Baadhi ya watumishi wa TSC Wilaya ya Mpwapwa wakiwa kwenye picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Idunda.

WADAU WA ELIMU WILAYANI HANDENI WASHIRIKI UTAFITI WA TSC

Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akizungumza na wadau wa elimu wilayani Handeni wakati wa ziara iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni kwa lengo la kukusanya maoni ya wadau wa elimu kwa njia ya madodoso ikiwa ni sehemu ya utafiti wa msingi (baseline Survey) unaolenga kujua hali ya utumishi wa walimu nchini.

Wadau wa Elimu wilayani Handeni wakimsikiliza Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa wakati wa ziara iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni kwa lengo la kukusanya maoni ya wadau wa elimu kwa njia ya madodoso ikiwa ni sehemu ya utafiti wa msingi (baseline Survey) unaolenga kujua hali ya utumishi wa walimu nchini.

MUUNGANO WA UPATIKANAJI CHAKULA SHULENI KUONGEZA AFYA YA AKILI NA MATOKEO YENYE TIJA KWA TAIFA

- Ni utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimu msingi;
- Fomu ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni yasainiwa;
- Kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga (kushoto) na Mkurugenzi Mkaazi Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson (Kulia) wakikabidhiana Fomu ya Makubaliano ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni baada ya kutia saini katika hafla iliyofanyika Jijini Dodoma.

Na. Mwandishi Wetu, Dodoma.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema kuwa ili kupata matokeo mazuri ya elimu ni lazima kuhakikisha upatikanaji wa lishe bora shuleni ili kuwajengea wanafunzi afya bora na kupata utulivu wa akili wawapo madarasani.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa hafla fupi ya Utiaji Saini Fomu ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni, Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omary Kipanga, alisema kuwa pamoja na kuwepo kwa Sera hiyo, utoaji wa huduma ya chakula shuleni umekuwa ukitekelezwa katika shule kwa namna na viwango tofauti.

Alisema katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, upatikanaji wa matokeo mazuri ya elimu hutegemea afya aliyonayo mwanafunzi huku Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ikifafanua upatikanaji wa huduma muhimu katika shule na vyuo ikiwemo huduma ya chakula bora, maji safi na salama na upatikanaji wa huduma za afya kwa wanafunzi.

"Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inafafanua kuhusu upatikanaji wa huduma muhimu katika shule na vyuo ikiwemo huduma ya chakula bora, maji safi na salama na upatikanaji wa huduma za afya kwa wanafunzi ndio maana kwa pamoja tunatia saini fomu ya kujiunga na

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga Akizungumza Jijini Dodoma wakati wa hafla fupi ya Utiaji Saini Fomu ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni.

MUUNGANO WA UPATIKANAJI CHAKULA SHULENI KUONGEZA AFYA YA AKILI NA MATOKEO YENYE TIJA KWA TAIFA

Baadhi ya wa Shiriki waliohudhuria hafla fupi ya Utiaji Saini Fomu ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni iliyofanyika Jijini Dodoma.

Muungano wa Chakula Shuleni nia ikiwa ni ileile ya kuhakikisha wanafunzi wanasoma vizuri na kupata matokeo mazuri." Alisema Mhe. Kipanga

Mhe. Kipanga alisema mwezi Oktoba, 2021 Wizara ya Elimu ilizindua Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimu Msingi ili kuweka utaratibu wa kitaifa ambao utawezesha wanafunzi kupata huduma hiyo muhimu.

"Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakinufaika na wengine kukosa huduma hiyo muhimu sasa naamini kupitia Muungano huu utasaidia kuziba yale mapengo yaliyokuwepo na wanafunzi sasa hawatakuwa na sababu yeyote ya kutopata matokeo mazuri," Alisema Mhe. Kipanga

Katika hatua nyingine, alisema kuwa utoaji wa huduma ya chakula na lishe shuleni ni suala mtambuka linalohitaji ushiriki wa sekta na wadau mbalimbali nakwa upande wa Tanzania, Muungano huu, ni jukwaa muhimu la kupata uzoefu wa namna nzuri ya kutekeleza mpango wa chakula shuleni kwa kushirikisha jamii na kufahamu wadau ambao tayari wapo kwenye muungano na wangependa kufadhili shughuli mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa chakula shuleni.

"Kujiunga na muungano huu kutawezesha wadau wetu wa maendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali, Makampuni binafsi pamoja na Vyombo vya Habari, kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa chakula na lishe shuleni," Alisema Mhe. Kipanga

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson, alisema kuwa moja ya njia ya kufikia malengo kwa Taifa lolote duniani ni lazima kuwekeza kwa watoto na hivyo ili kufikia huko lishe ni eneo linalohitaji maboresho makubwa.

Naye Mkuu wa Ofisi Ndogo ya Shirika la Mpango Chakula Duniani (WFP) Dodoma, Nima Sitta, alisema ni Muungano wa Kimataifa wa Chakula Shuleni ambao ni jukwaa la kuhakikisha nchi zote duniani ifikapo 2030 kila mtoto anapata angalau mlo mmoja shuleni.

Nao baadhi ya wanafunzi wakiwemo Beatrice Mtembi wa Shule ya Sekondari Dodoma na Lucas Mathias anayesoma Shule ya Msingi ya Mfano Chifu Mazengo kwa niaba ya Wanafunzi wengine nchini waliishukuru Serikali kwa hatua hiyo muhimu kwani itasaidia kuongeza ufaulu darasani na kuepuka vishawishi vitakavyosababisha kutotimiza ndoto zao.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe, akizungumza wakati wa hafla fupi ya Utiaji Saini Fomu ya kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni.

WAZIRI BASHUNGWA APIGA MARUFUKU WALIMU KUPITA KILA OFISI YA HALMASHAURI KUTAFUTA HUDUMA

Na. Mwandishi Wetu, Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Innocent Bashungwa amepiga marufuku walimu kupita kila Ofisi ya Halmashauri kutafuta huduma na ameagiza wapelekewe huduma hizo shuleni badala ya watoa huduma kufatwa ofisini.

Ametoa agizo hilo tarehe 8 Septemba, 2022 Jijini Dodoma wakati akiongea na waandishi wa habari kutoa taarifa kwa umma ya uboreshaji wa huduma kwa walimu nchini.

"Ni marufuku kuwaacha walimu kupita kila ofisi ya Halmashauri kutafuta huduma, narudia tena mwalimu apelekewe huduma shuleni badala ya watoa huduma kukaa ofisini" amesema Bashungwa

Amesisitiza kuwa Mwalimu akiandika barua kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhitaji huduma, anapaswa kujibiwa kwa maandishi ndani ya siku 7 baada ya kupokelewa.

Aidha, Bashungwa amewaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini kuwasimamia Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisaelimu, Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Wathibiti Ubora wa Shule kuhakikisha wanawafuata walimu shuleni na kutatua kero na malalamiko yao kwa wakati.

Amewataka viongozi hao kufuatilia na kuwasimamia viongozi wa elimu katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri, Kata na shule kutekeleza mikakati ya uboreshaji na usimamizi wa elimu na kuhakikisha wanawasilisha taarifa ya utekelezaji Ofisi ya Rais – TAMISEMI kila robo mwaka.

Vile vile, amewataka kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Mafunzo kazini kwa walimu, kwa mujibu wa Mwongozo uliotolewa na Katibu Mkuu Utumishi na ufanyike kwa uwazi na ushirishwaji wa kutosha, ili kuondoa dhana ya kuwa waajiri wanatoa nafasi za mafunzo kwa upendeleo.

Pia, Bashungwa amewaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwasimamia Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu kuzingatia miongozo ya upandishwaji vyeo walimu, ili kila anayestahili kupandishwa cheo, anapandishwa kwa mujibu Sheria, Kanuni na Miongozo.

SOPHIA MJEMA AWAONYA WALIMU KUKESHA VILABU VYA POMBE

Na. Mwandishi Wetu, Shinyanga.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema amekemea tabia ya baadhi ya walimu kukesha baa na kwenye vilabu vya pombe za kienyeji kila siku na kuwataka kurudisha hadhi ya walimu iliyokuwepo miaka ya nyuma nchini.

Akizungumza mkoani humo wakati wa uzinduzi wa vitabu vya mikakati ya kuboresha elimu nchini, Mjema amesisitiza kuwa hadhi ya walimu ambayo ilikuwepo miaka ya nyuma inapaswa kurejeshwa.

"Zamani ninakumbuka akipita mwalimu mtaani anaheshimika kweli, utasikia yule mwalimu fulani, hata akizungumza jambo kwenye mkutano linazingatiwa, lakini siku hizi heshima hiyo haipo tena, walimu wanalewa tu kwenye baa, wengine wanavaa nguo zisizo na staha yaani vurugu tupu," amesema Mjema.

WALIMU KUPEWA VISHIKWAMBI VYA SENSA YA WATU NA MAKAZI - NAIBU WAZIRI WA ELIMU JUMA KIPANGA

Na. Mwandishi Wetu, Dodoma.

"Serikali imesema mpango wa kugawa vishkwambi vilivyotumika katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi mwezi Agosti, 2022 kwa Walimu wote nchini kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji." Naibu Waziri wa Elimu, Omari Juma Kipanga.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknlojia, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga Bungeni Jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Hawa Subira Mwaifunga aliyetaka kujua mpango wa Serikali kueneza matumizi ya TEHAMA katika kufundisha ili kuwaokoa Walimu na matatizo ya mgongo na shingo.

UHAMISHO KWA WALIMU WAPYA WAPIGWA MARUFUKU NA MKUU WA MKOA NJOMBE

Na. Mwandishi Wetu, Njombe.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Anthony Mtaka amewaonya Walimu wa ajira mpya wenye matarajio ya kuomba uhamisho wa vituo vya kazi mara baada ya kupata ajira kuacha tabia hiyo.

Mtaka ametoa kauli hiyo kufuatia kitendo cha Watumishi wengi kuwa na tabia ya kuomba uhamisho mara baada ya kuona changamoto kwenye maeneo yao ya kazi.

Mtaka ametoa onyo hilo katika kikao cha uzinduzi wa vitabu vya mwongozo wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mkoa alipokutana na Walimu wapya wa mkoa huo katika Shule ya Sekondari Mpechi iliyopo Mjini Njombe.

“Ni lazima muangalie nyuma kwa shukrani na mjue kuna Maelfu ya wenye degree za elimu wamekosa kazi, sitarajii kuona mtu anahangaishana na Afisa Elimu kumwambia naomba nihamishie kituo fulani na Afisa Elimu usibebe dhambi ukiona simu yoyote mwambie nendeni kwa Mkuu wa Mkoa...”.

“Ni lazima muangalie nyuma kwa shukrani na mjue kuna Maelfu ya wenye degree za elimu wamekosa kazi, sitarajii kuona mtu anahangaishana na Afisa Elimu kumwambia naomba nihamishie kituo fulani na Afisa Elimu usibebe dhambi ukiona simu yoyote mwambie nendeni kwa Mkuu wa Mkoa, kama hautaki acha kazi uende kwenu.” Alisema RC Mtaka

RUKHSA WALIMU KUFUNDISHA WANAFUNZI KATIKA MUDA WA ZIADA KUPAISHA VIWANGO VYA TAALUMA – RC MTAKA

Na. Mwandishi Wetu, Njombe.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ametoa rukhsa kwa Walimu kufundisha Wanafunzi katika muda wao wa ziada ili kupandisha viwango vya taaluma katika Mkoa huo pamoja na kukuza vipato vyao.

Mtaka alitoa rukhsa hiyo katika kikao cha uzinduzi wa vitabu vya mwongozo wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mkoa bila kuvunja Sheria huku akidai kuwa haoni haja ya kuwazuia kuwa na ‘Tuition’ binafsi Walimu wakati kada nyingine wakiwemo Madaktari wamekuwa wakiongeza vipato vyao kwa kuwa na maduka ya dawa.

“Walimu wa Njombe unapomaliza muda wangu wa Serikali nenda kwenye ratiba yako binafsi ili tugawane namna ya kuwaondolea watoto ujinga kwenye vichwa vyao, fundisheni mimi nimewapa rukhsa, wakiwauliza waambieni RC ametoa rukhsa sio Afisa Elimu.” Alisema Mkuu huyo wa Mkoa wa Njombe

Mtaka alisema hataki kuona Mwalimu akifa maskini kwakuwa Madaktari wamekuwa na maduka ya dawa, zahanati na wanatibu zaidi ya hospitali mbili hivyo haoni haja ya kuwazuia walimu kuwa na ‘Tuition’ ili kujiongezea vipato vyao.

NATAMBUA UWEPO WA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) PEKEE HAPA NCHINI – RC MONGELLA

Na. Mwandishi Wetu, Mwanza

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amesema anatambua uwepo wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) pekee hapa nchini.

Kutokana na hali hiyo amewaonya baadhi ya maofisa wa Jiji la Arusha wanaopita kwenye shule mbalimbali Jijini hapo kutangaza kuhusu chama kingine cha walimu.

Mongella ameyasema hayo wakati akizindua miongozo mitatu ya uboreshaji wa elimu Mkoa wa Arusha.

Amesema baadhi ya Watumishi wa Jiji la Arusha, Idara ya Elimu wanapita kuhamasisha Walimu kujiunga na chama ambacho Serikali haikitambui.

Amesisitiza hataki migogoro mkoani kwake na kusisitiza Walimu kupendana, ikiwemo maofisa elimu kuacha kupanga safu za waratibu elimu kata au Wakuu wa Shule, wasiojua maana ya kuchafuka na chaki, kukosa viti au changamoto mbalimbali za walimu.

OFISI ZA TSC KYELA ZAFANYIWA UKARABATI

Mwonekano wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela Kabla ya kufanyiwa ukarabati.

Mwonekano wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela baada ya kufanyiwa ukarabati.

Mwonekano wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela Kabla ya kufanyiwa ukarabati.

Mwonekano wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela baada ya kufanyiwa ukarabati.

Mwonekano wa ndani wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela Kabla ya kufanyiwa ukarabati.

Mwonekano wa ndani wa Jengo la Ofisi za TSC Wilaya ya Kyela baada ya kufanyiwa ukarabati

OFISI ZA TSC WILAYA YA KOROGWE ZAFANYIWA UKARABATI

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe Agelina Msabaha akiwa ofisini kwake baada ya ofisi hiyo kufanyiwa ukarabati.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe Agelina Msabaha akizungumza jambo na Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa katika ofisi za TSC Wilaya ya Korogwe hivi Karibuni.



Mwonekano wa ndani wa ofisi za TSC Wilaya ya Korogwe baada ya kufanyiwa ukarabati.

WADAU WA ELIMU JIJI LA TANGA WASHIRIKI UTAFITI WA TSC

Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akiongea na wadau wa Elimu jijini Tanga waliokusanyika kwa lengo la kushiriki utafiti unaohusu masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu nchini.

Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa (katikati) akiwa pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanga, Naima Abtwalib (kushoto) wakisikiliza hoja za wadau wa elimu (hawapo pichani) jijini Tanga hivi karibuni.

Mmoja wa wadau wa elimu akizungumza katika kikao kifupi kujadili masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu mara baada ya kukamilisha kujaza madodoso ya utafiti unaohusu masuala ya utumishi wa walimu nchini.

Wadau wa Elimu jinini Tanga wakiwa kwenye kikao kifupi kujadili masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu mara baada ya kukamilisha kujaza madodoso ya utafiti unaohusu masuala ya utumishi wa walimu nchini.

TSC YASHAURIWA KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI WAKE, UZINGATIAJI WA TARATIBU KATIKA KUENDESHA MASHAURI YA NIDHAMU

Na. Mwandishi Wetu – Mbulu.

Wadau wa Elimu Wilayani Mbulu mkoani Manyara wameshauri TSC kuwajengea uwezo watumishi wake kuhusu taratibu za uendeshaji wa mashauri ya nidhamu ya walimu ili kuepuka kurudishwa kwa mashauri ili yaanzishwe upya pale walimu wanapokata rufaa Tume Makao Makuu kupinga uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya nidhamu ngazi ya Wilaya.

Ushauri huo umetolewa na wanadau mbalimbali wa elimu wilayani Mbulu wakati walipokutana na Maafisa kutoka TSC Makao Makuu waliofika wilayani hapo kwa lengo la kukusanya taarifa za utafiti kuhusu hali ya utumishi wa walimu nchini.

Akichangia mjadala, Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Bakari Urio alisema kumekuwa na rufaa mbalimbali za walimu zinazoamuliwa na TSC Makao makuu na kuelekezwa kuanza upya kwa shauri kutokana na kukiukwa kwa taratibu za uendeshaji wa mashauri hayo katika ngazi ya wilaya.

"TSC inatakiwa kujikita

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mbulu, Paschal Onna akizungumza na wadau wa elimu waliofika katika Ukumbi wa Mikutano wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilayani Mbulu kwa lengo la kujaza madodoso ya utafiti kuhusu hali ya utumishi wa walimu nchini.

Afisa Tarafa wa Tarafa ya Endagiikot wilayani Mbulu, Geofrey Nyumaizu akiongea kwa niaba ya Katibu Tawala wa Wilaya hiyo katika kikao kilichowakutanisha wadau wa Elimu wilayani Mbulu na Maafisa kutoka TSC Makao Makuu kilichofanyika wilayani hapo hivi karibuni.

Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Bakari Urio akizungumza wakati wa kikao kilichowakutanisha wadau wa elimu wilayani Mbulu na Maafisa kutoka TSC Makao Makuu kwa lengo la kujaza madodoso ya utafiti juu ya hali ya utumishi wa walimu nchini.

TSC YASHAURIWA KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI WAKE, UZINGATIAJI WA TARATIBU KATIKA KUENDESHA MASHAURI YA NIDHAMU

zaidi katika kutoa elimu kwa watendaji wake hasa katika eneo la uendeshaji wa mashauri ya nidhamu ya walimu. Uendeshaji wa mashauri ya walimu ni mchakato unaoendeshwa kisheria kwa asilimia mia moja, hivyo ni lazima taratibu zote zizingatiwe kama inavyoelekezwa. Kwa upande wa Wialaya yetu tumeona kuna nyakati mashauri yanarudishwa yaanze upya kwa kuwa hayakuzingatia sheria," alisema Urio.

Wadau hao pia walisema kuna haja kwa Serikali kuongeza bajeti ya TSC ili Tume hiyo iweze kutekeleza majukumu yake bila kikwazo au kuomba msaada kwenye Halmashauri ili hata inapokuja kwenye kufanya uamuzi iwe huru na isiegemee upande wowote.

Kwa upande wake Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa alisema kuwa Serikali imeamua kuboresha mazingira

Baadhi ya wadau wa elimu wilayani Mbulu waliohudhuria Kikao kilicholenga kupata taarifa za utafiti kuhusu hali ya utumishi wa walimu nchini.

ya walimu nchini kwa kuweka mifumo ya mawasiliano ambayo ni rahisi inayomfanya mwalimu asilazimike kuondoka kwenye kituo chake cha kazi kwa ajili ya kufuatilia masuala yake.

"Kwa upande wa TSC, kuna mfumo wa TSCMIS ambao utaanza kutumika hivi karibuni. Mfumo huo utamwezesha mwalimu kufuatilia masuala yake ya kiutumishi hata kwa kutumia simu yake ya mkononi. Mfumo huo ukianza utapunguza usumbufu kwa walimu kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi kwa ajili ya kufuata huduma," alisema Gwankisa.

Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akizungumza kwenye kikao kilichowakutanisha wadau wa elimu wilayani Mbulu kwa lengo la kupata taarifa za utafiti wa Msingi juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu.

Baadhi ya wadau wa elimu wilayani Mbulu waliohudhuria Kikao kilicholenga kupata taarifa za utafiti kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi wa Walimu.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania